**HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU**
**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 29/10/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI**

**MAHUDHURIO**

1. Bi. Mwanaisham Nassor – Mwenyekiti
2. Bw. Thomas Shilabu – Mjumbe
3. Bw. Thomas Shishwa - Mjumbe
4. Bi. Hadija Rajabu - Mjumbe
5. Joseph L.Hymu - Mjumbe
6. Bw. Said Kisamba - Mjumbe
7. Bw. Tito Joseph Mollel - Katibu

**SECRETARIET**

1. Rehema Tito Yangayanja – Kitengo cha Manunuzi

**AGENDA:**

1. Kufungua Kikao
2. Kupitia na nakuridhia agenda
3. Kupitisha njia ya Manunuzi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopo kwa mwaka wa fedha 2021-2022
4. Mengineyo Kwa Idhini ya Mwenyekiti
5. Kufunga Kikao.

**AGENDA NA.01/10/BZ 2021 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5:25 Mchana kwa kuwasalimu wajumbe wa bodi ya zabuni kwa kuendelea kutetekeleza majukumu ya bodi ya zabuni kwa ushirikiano na kwa Mujibu wa sheria.Mwenyekiti aliwajulisha kuwa kikao ni cha robo ya pili kwa mujibu wa kalenda.

**AGENDA NA.02/10/BZ 2021. KUPITIA NA KURIDHIA AGENDA**

Agenda zilizowasilishwa ndizo zilizokubalika kujadiliwa hapakuwa na marekebisho ya agenda

**AGENDA.NA.03.10.BZ.2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 27.05.2021**

Muhtasari wa tarehe 27.5.2021 ulisomwa na kuthibitishwa kwa kusainiwa na katibu na Mwenyekiti kuwa kumbukumbu halali kwa mujibu wa sheria ya manunuzi na uendeshaji wa vikao.

**AGENDA.NA.04.10.BZ.2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 27.05.2021**

Taarifa ya Utekelezaji wa maazimio yaliwasilishwa na wajumbe walipokea kama ifuatavyo:

1. Kuhusu Utekelezaji wa Ujenzi wa Dhahanati za Mwanyahina, Sapa, Makomangwa na Mwandukisesa-Iliazimia kuwa fedha zilizopokelewa Tshs.200,000,000 zitumike kukamilisha ujenzi wa zahanati

**UTEKELEZAJI**

Maelekezo yametolewa katika kamati za Ujenzi na Mapokezi kuhakikisha fedha zilizopokelewa zinajenga na kukamilisha majengo ya ODP ndipo shughuli za ujenzi wa vyoo matundu mawili,Kichomea taka na Incenerator zipewe kipaumbele

Zahanari ya Makomangwa imekamilika jingo la OPD,Vyoo matundu Manne,Kichomea taka, incenerata, Fedha zilizobaki serikali ya kijiji zimeomba kuanza ujenzi wa Nyuma ya mtumishi (3.6m)

Zahanati ya Mwanyahina Wamekamilisha Ujenzi wa ODP,Ujenzi wa Matundu ya vyoo unaendelea,hata hivyo kumekuwa na changamoto ya uchimbaji wa matundu ya vyoo,

Ujenzi wa Zahanati ya Mwandukisesa jengo la ODP wanamalizia ufungaji wa umeme na fedha zao zimeisha

Kuhusu zahanati ya Sapa,Jengo limeishia hatua ya dari na ripu kwani fedha zao zimekwisha hivyo wanampango wa kuendelea na ujenzi watakapopata fedha za Hifadhi.

**AGENDA NA.05/10/BZ 2021 KUPITISHA NJIA YA MANUNUZI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021-2022**

Katibu aliwasilisha taarifa ya miradi iliopokea fedha ili wajumbe wajadili na kutolea maamuzi ya njia za manunuzi itakayotumika kama ifuatavyo:

- ✓ **IDARA YA ELIMU SEKONDARI NA MSINGI**

| Jina La Mradi | Kiasi kilichopokelewa | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Madarasa mawili shule ya sekondari Lyusa | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya SekondariNg'hoboko | 20,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Meatu | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwanjolo | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Kimali | 60,000,000 | UVIKO |

| | | |
|---|---|---|
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Makao | 20,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwamishali | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwamanongu | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwamamole | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Nyalanja | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Paji | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Imalaseko | 20,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Bukundi | 20,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Saka Saka | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Lingeka | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwandoya | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwakaluba | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwakisandu | 20,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwabusalu | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwabuma | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Lubiga | 80,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Mwaukoli | 20,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Kisesa | 60,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule ya Sekondari Itinje | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa darasa Moja shule Shikizi Mwasungura | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa Madarasa Shule shikizi Mwajimoso | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa Madarasa Shule shikizi Mwababili | 80,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa Madarasa Shule shikizi Mwajimoso | 40,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa Madarasa Shule shikizi kasala | 120,000,000 | UVIKO |
| Ujenzi wa Madarasa Shule shikizi mwashigela | 40,000,000 | UVIKO |
| JUMLA KUU | 1,120,000,000/= | |

**IDARA YA AFYA**

| Jina La Mradi | Kiasi kilichopokelewa | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Kituo cha afya Tarafa ya Kimali katika kijiji cha Iramba Ndogo | 250,000,000 | Serikali Kuu |

Kitengo cha Manunuzi kiliwasilisha mapendekezo ya kutumia njia ya manunuzi ya force account na kutoa sababu zifuatavyo.

1. Njia hii ni rahisi kutumika kwani miradi inayotekelezwa ipo chini ya uwezo wa wataalam wa Halmashauri katika usimamizi
2. Miradi hii ipo Maeneo ya vijijini hivyo njia ya force account ni shirikishi kwa wananchi.

3. Njia hii ya manunuzi ipo kwa mujibu wa sheria na inatoa fursa ya kununua vifaa viwandani, kwa wananchi kupata fursa ya ajira hivyo ni vema kutumika.

Katibu wa bodi ya zabuni aliwajulisha wajumbe juu ya muundo wa utekelezaji wa miradi ngazi ya wilaya na ngazi ya kituo kama ifuatavyo;

| ***Maelezo ya Kipengele*** | ***Mhusika Mkuu*** |
|---|---|
| Makadirio/Makisio za Gharama za Ufundi na vifaa vya Ujenzi (Schedule of Materials | Mhandisi wa Wilaya kuandaa na kuwapatia idara husika kwa ajili ya utekelezaji katika lower level |
| Mpango Kazi wa Utelezaji wa Mradi | Mhandisi |
| Quality Assuarance & Control Plan/Strategy | Kamati za Ufuatiliaji,Mkoa,Wilaya na Wizara |
| Value for Money Attainment &Cost Control plan | Kamati za Ufuatiliaji |
| Mihtasari ya Kamati za Ujenzi na Kamati ya Manunuzi ununuzi wa vifaa na ufundi | Ngazi ya kituo |
| Mikataba ya Mafundi na Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi | Ngazi ya kituo- Upekuzi kufanyika kupitia ofisi ya Mwanasheria |

Baada ya kupitia Mapendekezo na vipengele vyote wajumbe waliridhia na kutoa Maamuzi yafuatayo;

1. Ofisi ya Mhandisi wa Ujenzi iandae Makisio ya Gharama ya Vifaa na Ufundi kwa kila mradi kulingana na bajeti na Kuwasilisha katika idara Husika
2. Kila Idara zenye bajeti kwa Kushirikiana na Kitengo cha Ununuzi na Ugavi Kuhakikisha Kamati zinaundwa na Kutekeleza Majukumu yake

Njia za Manunuzi ya Bidhaa zitakazotumika.

- Ununuzi wa bidhaa zisizo za viwandani kutoka kwa jamii husika (Wasomba Mchanga,Kokoto na Mawe) Locally availability from the community.
- Ununuzi wa Bidhaa za viwandani – Njia Mbali mbali zitatumika ikiwa ni pamoja na Single Source,Ushindanishi wa wazabuni, Manunuzi ya Moja kwa Moja (Kutoka viwandani au kwa mawakala wa viwanda) kwa Mujibu wa Muongozo wa PPRA.

**MWISHO**

Bodi ya zabuni iliridhia kutumika kwa njia ya force account na kusisitiza umuhimu wa usimamizi wa karibu kwani miradi hii ni ya kimkakati na imetolewa ukomo wa ukamishaji kitaifa.

**AGENDA NA.06/10/BZ 2021 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hapakuwa na Mengineyo yaliowasilishwa kwaajili ya kujadiliwa

**AGENDA NA.07/10/BZ 2021 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 8:13 Mchana na kusisitiza ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo wa utaratibu wa maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwani kwa robo ya kwanza ingepaswa miradi hii ianze kutekelezwa.

Imethibitishwa Na

..............................

**Ndg. Mwanaisham Nassor Mollel**

**Mwenyekiti**

..............................

**Ndg. Tito Joseph**

**Katibu**

**Tarehe** 17/12/2021

......................xxxxxxxxxxxxxxxx....................................